" Hekima ni mti wa Uzima"

# Kitabu Cha Mzazi

Hiki ni kitabu kinachotoa maelezo mafupi kuhusu shule ya Tree of Life. Kitabu hiki kinaeleza baadhi ya miongozo katika shule na pia kinaweza kufanyiwa mabadiliko wakati wowote.

**Tree of Life School**
**P.O. Box 269, Magu**
**0753 629 821**

www.treeoflifetanzania.org

<u>YALIYOMO</u>

YALIYOMO ............ 2
MAONO YETU ............ 3
DIRA YETU ............ 3
KAULI MBIU ............ 3
MSTARI MKUU ............ 3
MAADILI YETU ............ 3
WALIMU WA SHULE ............ 4
TAARIFA MUHIMU KUHUSU SHULE ............ 4
MAHITAJI MUHIMU YA MWANAFUNZI ............ 4
MAELEZO YA JUMLA ............ 5
KUINGIA SHULE NA KUTAWANYIKA ............ 5
MAHUDHURIO YA WANAFUNZI ............ 5
KUTOKUFIKA SHULE ............ 5
UCHELEWAJI ............ 5
UTORO ............ 6
KURUDIA DARASA ............ 6
MALIPO YA ADA ZA SHULE ............ 6
NIDHAMU YA WANAFUNZI ............ 7
SARE ZA SHULE ............ 7
TABIA YA WANAFUNZI ............ 7
ADHABU ZINAZOWEZA KUTOLEWA ............ 8
SHERIA ZA GARI LA SHULE ............ 8

**MAONO YETU**
Kuwa na jamii ya wanafunziambao wanaweza kutumia elimu ya darasanina ujuzi wa kibiblia kwa maisha yao ya kila siku

**DIRA YETU**
Kuwapa wanafunzi wetu fursa ya kujifunza katika ubunifu na vitendo, pia kuhusisha ukweli wa biblia katika kila nyanja shuleni

**KAULI MBIU**
"Hekima ni Mti wa Uzima" (Mithali 3:18)

**MSTARI MKUU**
Ufunuo 22:1-2: Kisha yule malaika akanionyesha mto wa maji ya uzima ung'aao kama kioo na kutiririka kutoka kwenye kiti cha enzi cha Mungu na cha Mwana-Kondoo, kupitia katikati ya barabara kuu ya mji huo. Katika pande zote za mto huo kulikuwa na mti wa uzima utoao matunda ya aina kumi na mbili, na kuzaa matunda yake kila mwezi. Majani yake ni ya kuwaponya watu wa mataifa.

**MAADILI YETU**

- **Uadilifu** – Tunaamini Neno la Mungu.Tunaamini katika kufanya yaliyo sahihi hata kama hakuna anayetuona. Tunaamini katika kumuheshimu Mungu zaidi ya kitu chochote.
- **Upendo** – Tunathamini watoto.Tunaamini katika kumpenda mwingine kama tunavyojipenda.Tunaamini uwezo wa upendo wetu unatoka kwa Mungu.
- **Familia** – Tunathamini familia.Tunaamini katika kushirikiana na wazazi.Tunaamini watoto hujifunza nyumbani pia, sio shuleni tu.
  **Ubunifu** – Tunathamini elimu ya vitendo.
  Tunaamini katika kujaribu vitu vipya.Tunaamini kujifunza kunaweza kuburudisha.
- **Heshima** – Tunathaminiana.Tunaamini katika kuheshimu muda wa wengine.Tunaamini tunaweza kujifunza kutoka kwenyemawazo, lugha na tamaduni za wengine.

## WALIMU WA SHULE

| Jina la mwalimu | Namba ya simu |
|---|---|
| Mwalimu Mkuu: Elifurah Masega | 0621632870 |
| Mwalimu Mkuu Msaidizi: Milka Mbugua | 0743297247 |
| Mwalimu wa Chekechea: Rachel Moses | 0742937365 |
| Mwalimu wa Darasa la Kwanza: Salima Sanga | 0759350106 |
| Mwalimu wa Darasa la Pili: Tunda Silas Mella | 0764464448 |
| Mwalimu wa Darasa la Tatu: Nestory Paul | 0756546925 |
| Mwalimu wa Darasa la nne: Kessy Philbert | 0628989615 |
| Mwalimu wa Darasa la Tano: Mrisho Masolwa | 0744454102 |
| Mwalimu wa Darasa la Sita: Paul W. Everist | 0746842765 |
| Mwalimu wa Darasa la Saba; Elifurah Masega | 0621632870 |

## TAARIFA MUHIMU KUHUSU SHULE

1. Shule yetu ni ya Kikristo.
2. Shule inafuata mihula iliyoidhinishwa na Ofisi ya Raisi TAMISEMI.
3. Shule hii ni ya kutwa.
4. Shule inatoa huduma ya chakula.
5. Wanafunzi wanaingia shule saa 1:30 asubuhi na kutoka saa 10:30 jioni.
6. Lazima wanafunzi wawe na umri wa kuanzia miaka 5 kwa chekechea na kuanzia miaka 6 kwa darasa la kwanza.
7. Kila darasa linatakiwa kuwa na idadi ya wanafunzi wasiozidi 25.
8. Shule haiwapokei wanafunzi wenye mahitaji maalumu kwa sasa kwa makundi yafuatayo: vipofu, viziwi, na wenye matatizo ya akili.
9. Huduma ya usafiri inapatikana shuleni.

## MAHITAJI MUHIMU YA MWANAFUNZI

1. Cheti cha Kuzaliwa
2. Vifaa vya Darasani

   *Chekechea:*
   - Begi la kubebea madaftari (1)
   - Spring file (2)

   *Darasa la kwanza, la pili, na la tatu:*
   - Begi la kubebea madaftari (1)
   - Madaftari ya kawaida (5)
   - Madaftari ya hesabu (2)
   - Madaftari ya mwandiko (2)
   - Spring file (1)

**KUMBUKA:** Ni wajibu wa mzazi/mlezi wa mwanafunzi kumnunulia mwanafunzi madaftari. Iwapo yataisha, atapewa taarifa kununua mengine.

## MAELEZO YA JUMLA

## KUINGIA SHULE NA KUTAWANYIKA

- Wanafunzi wanatakiwa kufika shule saa moja na nusu asubuhi.
- Muda wanafunzi kutawanyika ni saa kumi na nusu jioni kwa siku za Jumatatu hadi Alhamisi.
- Muda wanafunzi kutawanyika ni saa tisa na nusu alasiri siku ya Ijumaa.

## MAHUDHURIO YA WANAFUNZI

- Ni wajibu kwa kila mwalimu wa darasa kuita majina ya wanafunzi kila sikuna kuyapeleka kwa mwalimu mkuu kwa ajili ya kuhakiki.
- Ikiwa mwanafunzi hatakuja shule, mwalimu wa darasa atawasiliana na mkuu wa shule.
- Mwalimu mkuu atawasiliana na mzazi au mlezi ili kujua kwa nini mwanafunzi hajafika shule.
- Gari linaondoka Nyanguge saa moja kamili asubuhi kuelekea shule, na linafika Nyanguge saa kumi na moja kamili jioni kutoka shule, isipokuwa Ijumaa linafika saa kumi kamili jioni.

## KUTOKUFIKA SHULE

- Kuna aina mbili za kutokufika shule: utoro na ruhusa. Mwanafunzi atapewa ruhusa ya kutokufika shule kwa sababu hizi: ugonjwa ikiwa umethibitishwa na mzazi au mlezi, msiba wa mzazi, ndugu wa damu, bibi au babu,au mazingira hatarishi kwa mwanafunzi. Sababu zingine zitakubaliwa na shule ikiwa mzazi au mlezi atamwombea mwanafunzi ruhusa.
- Ikiwa mwanafunzi hawezi kufika shule, mzazi au mlezi anatakiwa kutoa taarifa shuleni kabla ya saa mbili kamili asubuhi.
- Ikiwa mzazi hajatoa taarifa kabla ya saa mbili kamili, mwalimu atampigia mzazi au mlezi kumuuliza kwa nini mwanafunzi hajafika shule.
- Ikiwa mwanafunzi hatafika shule bila sababu, atawajibika.

## UCHELEWAJI

- Kufika shuleni kwa wakati ni muhimusana, ili kupata muda wa kutosha kwa shughuli za darasani na kupunguza usumbufu darasani.
- Uchelewaji wa mwanafunzi shuleni unaweza kupelekea akapata adhabu.
- Ikiwa mwanafunzi atachelewa mara kwa mara, shule itawasiliana na mzazi au mlezi wa mwanafunzi ili kujadiliana jinsi ya kumsaidia mwanafunzi ili aweze kufika kwa wakati.

**UTORO**

- Ikiwa mwanafunzi atakosa masomo kwa muda wa wiki mbili au Zaidi mfululizo atatakiwa kuwa na masomo ya ziada (tuition) na mzazi atawajibika katika hilo.
- Ikiwa mwanafunzi atakosa masomo kwa miezi mitatu mfululizo ataondolewa shuleni, au atarudia darasa mwaka unaofuatia.

**KURUDIA DARASA**

- Mwishoni mwa mwaka mwalimu wa darasa atapima maendeleo ya mwanafunzi, ili kujiridhisha kama mwanafunzi yuko tayari kuendelea na darasa linalofuata. Kwa mwanafunzi atakayeonekana anauhitaji wa kurudia darasa, lazima kuwa na makubaliano ya walimu pamoja na wazazi wa mwanafunzi.
- Ikiwa mwanafunzi atatakiwa kurudia darasa, mzazi/mlezi wake ataandika barua kwenye ofisi za elimu wilaya akieleza sababu za kurudia darasa. Maombi hayo yanaweza kukubaliwa au kukataliwa.
- Kwa tatizo la utoro uliopitiliza, mwanafunzi atarudia darasa kutokana na sheria zilizowekwa na wizara ya elimu.

**MALIPO YA ADA ZA SHULE**

1. Malipo yote ni lazima yafanyike kabla ya muhula husika kufunguliwa.
2. Ada za shule zitakuwa 800,000/= kwa mwaka. Hii ni pamoja na gharama za chakula. Tunapokea kwa awamu zisizozidi tatu kama inavyoonekana hapo chini.

| Jumla ya Ada kwa Mwaka (*Darasa la Kwanza mpaka la Saba)* | Malipo #1 Lazima yalipwe siku ya kwanza ya mhula wa kwanza (au kabla). | Malipo #2 Lazima yalipwe siku ya kwanza ya mhula wa pili (au kabla). | Malipo #3 Lazima yalipwe siku ya kwanza ya mhula wa tatu (au kabla). |
|---|---|---|---|
| 800,000 | 400,000 | 200,000 | 200,000 |
| Jumla ya Ada kwa Mwaka *(Darasa la Awali)* | | | |
| 500,000 | 200,000 | 200,000 | 100,000 |

3. Gharama ya usafiri kwa madarasa yote ni TSH 400,000/= kwa mwaka.
4. Malipo yote yatafanyika katika benki ya **CRDB**, jina la account **TREE OF LIFE SCHOOL**, account no. **0150518774200**.
5. Gharama iliyokwisha kulipwa kwa ajili ya ada haitarudishwa.
6. Malipo mengine ni kama ifuatavyo:
    - Ada ya uandikishwaji wa mwanafunzi: 10,000/=
      *Haya malipo ni kwa mwanafunzi mpya anayejiunga na shule ya Tree of Life.*
    - Fedha ya Tahadhari: 20,000/=
      *Hizi gharama zitatumika kufidia uharibifu wa kusudi utakaofanywa na mwanafunzi. Iwapo mwanafunzi atatumia fedha zote za tahadhari, mzazi/mlezi atalazimika kulipa fedha nyingine kwa ajili ya tahadhari.*
    - Fedha ya Tahadhari ya Vitabu: Tsh 10,000/= kwa kila kitabu kimoja

*Hii fedha imebeba gharama za vitabu vya mwanafunzi atakavyovitumia shuleni na nyumbani. Hizi fedha zitarudishwa kwa mzazi/mlezi mwishoni mwa mwaka iwapo vitabu vyote vitarudishwa vikiwa katika hali nzuri.*

- Ada lazima ilipwe siku ya kwanza ya muhula; tofauti na hapo mwanafunzi hatapokelewa.
- Siku ambazo mwanafunzi hatakuwa shuleni sababu ya ada itahesabika kama utoro.
- Ikiwa mwanafunzi atakosa masomo kwa muda mrefu kutokana na kutokulipa ada, itambidi ahudhulie masomo ya ziada (tuition) na mzazi atajibika.
- Mwanafunzi ambaye hatalipa ada, anaweza kupoteza nafasi yake na kuchukuliwa na mwafunzi mwingine.
- Ikiwa ada italipwa kwa kuchelewa (baada ya usajili) mzazi atalazimika kumsajili upya mwanafunzi Pamoja na kulipia fomu ya uandikishaji.

## NIDHAMU YA WANAFUNZI

## SARE ZA SHULE

- Sare za Shule
    - Kwa wavulana: shati jeupe aina ya Tomato lenye kola na mikono mifupi, kaptura nyeusi, soksi nyeupe, viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba
    - Kwa wasichana: shati jeupe aina ya Tomato lenye kola na mikono mifupi, sketi nyeusi, soksi nyeupe, viatu vyeusi vya ngozi venye kamba ama visivyo na kamba, pia visivyo na visigino virefu
    - Kwa michezo: viatu vya michezo vyenye rangi ya aina yoyote ile
    - Sare zitakazopatikana shuleni: sweta na tisheti za shule; kila mwanafunzi atatakiwa kuwa na sweta na tisheti kuanzia moja. Mwanafunzi hawatakiwi kuvaa sweta ambalo sio la shule akiwa shuleni.
    - SKETI: lazima ziwe chini ya magoti na zishonwe na kaptura kama inavyoonyeshwa



**KUMBUKA:** Ni wajibu wa mzazi/mlezi wa mwanafunzi kumnunulia mwanafunzi sare za shule.

- Wanafunzi lazima wavae sare za shule kila siku wawapo shuleni.
- Kila mwanafunzi lazima anyoe nywele zake (kianafunzi).
- Ikiwa mwanafunzi atafika shuleni bila sare kamili ya shule ama bila kunyoa nywele, hatarudishwa nyumbani bali atawajabika.

## TABIA YA WANAFUNZI

- Tunatarajia wanafunzi wote kufuata sheria, kanuni na taratibu za shule.

- Wanafunzi wanatakiwa kupunguza kelele wawapo darasani.
- Wanafunzi wanatakiwa kuheshimiana na kuwaheshimu wote wanaowazunguka bila kujali umri, dini au kabila.
- Wanafunzi lazima wapate ruhusa kutoka kwa mwalimu ya kuingia na kutoka darasani, mfano: kwenda chooni, bwaloni, n.k. Hawaruhusiwi kutembeatembea bila ruhusa.
- Wanafunzi wanatakiwa kutembea na sio kukimbia wanapotoka sehemu moja kwenda nyingine (hususani kwenye veranda la shule).

**ADHABU ZINAZOWEZA KUTOLEWA**

- Hizi ni baadhi ya adhabu anazoweza kupata mwanafunzi:
    - Kuonywa kwa maneno kutoka kwa mwalimu
    - Mazungumzo na mwalimu
    - Atapata nafasi ya kuomba msamaha
    - Kumpeleka kwenye ofisi za mkuu wa shule
    - Kutokufanya jambo analolipenda (mfano,kutokucheza muda ma mupumziko)
    - Kuwasiliana na wazazi/walezi
    - Kukaa peke yake ama mbali na rafiki zake
    - Kusafisha mazingira
    - Kazi zaidi ya kufanya darasani au nyumbani

Mkuu wa shule au mkuu msaidizi wa shule tu ndio wanaoruhusiwa kutoa adhabu ya viboko kwa mwanafunzi

**SHERIA ZA GARI LA SHULE**

- Shule ya Tree of Life inatoa huduma ya usafiri kwa wanafunzi waliolipia huduma ya usafiri.
- Fedha ya usafiri ni lazima ilipwe siku ya kwanza ya muhula; tofauti na hapo mwanafunzi hataruhusiwa kutumia gari la shule.
- Mwanafunzi anapokuwa kwenye gari la shule anakuwa chini ya viongozi wa shule, ambapo dereva anayo mamlaka ya kutoa taarifa ya utovu wa nidhamu wa mwanafunzi (aliofanya ndani ya gari) kwenye uongozi wa shule.
- Mwanafunzi anatakiwa kufuata sheria za shule anapokuwa ndani ya gari la shule. Mwanafunzi anaweza kusimamishwa kutumia gari la shule ikiwa atavunja kanuni na sheria za gari la shule pamoja na sheria za shule, mfano:
    - Kuvunja sheria na taratibu za shule
    - Kumuumiza au kutishia kumuumiza dereva au yeyote anayetumia gari la shule
    - Kufanya uharibifu kwenye gari la shule kwa makusudi au zaidi ya mara moja
    - Kutokumuheshimu dereva, msimamizi wa gari, au mwanafunzi mwenzake